JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

# MWONGOZO WA KUSHIRIKISHA SEKTA BINAFSI

JULAI, 2020

# Yaliyomo

VIFUPISHO ..... iii
1. UTANGULIZI ..... 1
2. HALI YA HUDUMA NA USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI ..... 1
3. LENGO LA MWONGOZO ..... 2
4. USHIRIKISHAJI WA WATOA HUDUMA BINAFSI ..... 3
5. VIGEZO VYA USHIRIKISHAJI ..... 3
6. HATUA ZA KUFUATA ..... 5
7. MAJUKUMU YA MSIMAMIZI HUDUMA ..... 6
8. MATARAJIO NA VIWANGO ..... 8
9. HAKI ZA MSIMAMIZI HUDUMA ..... 9
10. WAJIBU NA HAKI ZA RUWASA ..... 9
11. MAJUKUMU NA HAKI ZA JUMUIYA ..... 11
12. UKOMO WA MWONGOZO ..... 11
13. KUPITISHWA ..... 11

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | CBWSOs | Community Based Water Supply Organizations (Jumuiya za watoa huduma za maji katika Jamii) |
| 2. | NAWAPO | National Water Policy (Sera ya Maji ya Taifa) |
| 3. | OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| 4. | RUWASA | Rural Water Supply and Sanitation Agency (Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini) |

## 1. UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania inatekeleza Programu ya Sekta ya Maji kwa awamu. Awamu ya kwanza ilianza mwaka 2005/6 na kumalizika Juni 2016. Awamu ya pili ambayo ndio inayotekelezwa hadi sasa ilianza kutekelezwa Julai 2016. Usimamizi wa utekelezaji wa Programu unaratibiwa na Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara za TAMISEMI, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee Watotona Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia.

Kuanzia Julai 2019, Serikali imefanya mabadiliko ya mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira. Katika mabadiliko hayo, Wizara ya Maji imepewa mamlaka ya kusimamia sekta kwa ujumla wake ikiwa ni pamoja na watumishi wote wa huduma za maji nchi nzima kuhamishiwa Wizara ya Maji ambayo itawasimamia kiutaalam, kiutawala na kinidhamu.

Mabadiliko haya yamehitimishwa kwa utungaji wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira na. 5 ya mwaka 2019. Sheria hii ndio iliyoanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), taasisi mahsusi kwa ajili ya kusimamia huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini. RUWASA imekasimiwa mamlaka ya kusanifu, kujenga, kusimamia na kuendeleza miundombinu na huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Katika ngazi ya jamii, RUWASA imepewa nguvu kisheria kusimamia uendeshaji wa Jumuiya za Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) ambazo zimepata sura mpya ya kisheria katika muundo na uendeshaji wake. Sheria mpya inataka Jumuiya zote ziendeshwe kitaalamu na Timu ya Uendeshaji yenye wajumbe wenye utaalam katika masuala ya ufundi na fedha na wakati huo huo imepanua uwigo wa usimamizi kwa kuingiza wajumbe wa Kamati za Maji kutoka katika ngazi na kada mbalimbali kuanzia Kijiji, Kata, Halmashauri na Wilaya.

## 2. HALI YA HUDUMA NA USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI

Kiuendeshaji, takwimu zinaonyesha kuwa kumefanyika uwekezaji mkubwa sana katika miradi ya maji katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji nchi nzima na hasa vijijini. Taarifa zinaonyesha kuwa pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanyika, upatikanaji wa Maji safi bado imekuwa ni tatizo kwa sababu ni theluthi mbili tu ya Vichoteo na Virula vilivyojengwa ndio vinafanya kazi. Hali hii imetokana na sababu kadhaa za kiufundi, kiuendeshaji, kiutawala na kifedha.

Sababu mojawapo ya tatizo la upatikanaji wa maji safi ni kutenga fedha kidogo sana kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya maji na uimarishaji taasisi katika sekta ya maji. Sababu hii imechangiwa na utaratibu uliokuwa unatumika kutenga fedha za miradi katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Sekta Maji ambapo bajeti ya uendeshaji na matengenezo ilipewa umuhimu mdogo.

Sababu nyingine kubwa ni ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika Uendeshaji na Matengenezo ya miradi ya maji. Utamaduni uliojengeka ni kuwa sekta binafsi inashiriki katika ujenzi tu na kuacha uendeshaji na matengenezo katika mikono ya wananchi kupitia Jumuiya za Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii. Bahati mbaya ni kuwa Jumuiya zimekuwa zikiendeshwa na wananchi ambao asilimia kubwa hawana elimu wala utaalam wa kusimamia huduma, kuendesha taasisi wala kufanya biashara.

Aidha, ingawa Sera ya Maji (NAWAPO) ya mwaka 2002 na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 vimetilia mkazo ushirikishaji wa sekta binafsi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji katika ngazi zote, lakini bado uhalisia kwenye utekelezaji ni kinyume chake.

Ushirikishaji mdogo wa Sekta binafsi katika uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji umeikosesha sekta fursa ya kufaidika na ujuzi na uzoefu wa ujasiriamali ambao ungeongeza tija na ubora katika usimamizi wa huduma na usimikaji wa taasisi katika ngazi ya jamii.

Kwa kutambua udhaifu huo katika ushirikishaji wa Sekta binafsi kwenye uendeshaji na matengenezo, RUWASA imeandaa Mwongozo wa kuchagiza ushiriki na kuainisha vigezo vya kufikia uamuzi na hatua za kufuata kwenye mchakato wa kushirikisha watoa huduma binafsi katika huduma ya maji ngazi ya Jamii.

## 3. LENGO LA MWONGOZO

Mwongozo huu unalenga kutoa maelekezo na ufafanuzi kuhusu utaratibu na hatua za kufuata kwenye ushirikishaji wa sekta binafsi katika Huduma za Maji Ngazi ya Jamii. Msisitizo umewekwa kwenye vigezo muhimu vya kuzingatia katika kufikia maamuzi na hatua mahsusi zilizoainishwa kisheria katika mchakato mzima wa kushirikisha Watoa huduma binafsi.

## 4. USHIRIKISHAJI WA WATOA HUDUMA BINAFSI

Dhana ya kushirikisha watoa huduma binafsi kutoka sekta binafsi imejengwa kwenye matarajio kuwa kuna maeneo muhimu ya uendeshaji wa Jumuiya za Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii ambayo yakipata vionjo vya sekta binafsi kunakuwa na mageuzi makubwa katika viwango vya uendeshaji wa taasisi na ubora wa huduma zinazotolewa. Maeneo ya kimkakati katika ushirikishaji wa sekta binafsi kuimarisha ufanisi wa taasisi na huduma ni;

(a) **Uendeshaji na Matengenezo:** Usimamizi wa kila siku wa huduma na ufanyaji kazi wa mashine, mitambo na miundombinu. Hii inajumuisha ukarabati na marekebisho ya pampu, jenereta, mabomba na Dira za Maji.

(b) **Ukusanyaji Mapato:** Kuandaa Ankara na kukusanya malipo, tozo, ada na madeni yote ya Jumuiya. Eneo hili linajumuisha mfumo maalum wa kuhifadhi taarifa za fedha kwa uwazi na kwa utaratibu unaokubalika na unaoweza kukaguliwa na wataalamu wa RUWASA

(c) **Ukarabati, upanuzi na vipuri:** Utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya matengenezo na ukarabati mkubwa katika miundombinu ya uzalishaji na utoaji huduma.

(d) **Mipango na Bajeti:** Mtoa huduma kusaidia utayarishaji wa Mpango na Bajeti na uhuishaji wa CBWSOs.

## 5. VIGEZO VYA USHIRIKISHAJI

Kabla ya kufikia maamuzi na kuingia katika makubaliano ya kushirikiana na Sekta binafsi, Jumuiya zitazingatia yafuatayo;:-

(a) Umiliki wa miundombinu yote ya uzalishaji na usambazaji wa maji utabaki kwa Serikali na Wananchi bila kujali ni nani anayesimamia au kuendesha utoaji wa huduma wakati husika.

(b) Makubaliano yote ya ushirikishaji wa sekta binafsi yatakuwa kati ya Jumuiya husika na Msimamizi Huduma/Mtoa Huduma kwa kibali cha RUWASA na ushauri wa Halmashauri husika

(c) Kutegemeana na mahitaji, Jumuiya inaweza kushirikiana na sekta binafsi kwa makubaliano na Msimamizi Huduma au Mtoa Huduma:-

   (i) Msimamizi Huduma anawajibika kwa mambo yote ya uzalishaji na usambazaji wa Huduma ikiwa ni pamoja na ukusanyaji na utunzaji wa maduhuli, malipo ya asilimia kama walivyokubaliana kwa Jumuiya husika na matengenezo ya kawaida ya mitambo/miundombinu ya huduma.

(ii) Mtoa Huduma anawajibika kwa eneo au baadhi ya maeneo ya huduma ambayo yameainishwa kwenye makubaliano kutokana na mahitaji ya Jumuiya kwa wakati husika kama vile matengenezo, mafunzo na vipuri.

(d) RUWASA ndiye mdhamini mkuu wa makubaliano yote yanayofikiwa kati ya Jumuiya na Sekta Binafsi na ndiye mthamini na mwangalizi wa mahusiano kati Jumuiya na Sekta binafsi.

(e) Kabla ya kuamua kushirikisha sekta binafsi Jumuiya lazima ishauriane na RUWASA na kujiridhisha kuwa hali ya uendeshaji na utoaji wa huduma hairidhishi na kuwa suluhisho la hali hiyo linaweza kupatikana kwa kushirikisha sekta binafsi.

(f) Jumuiya lazima ifanye tathmini kwa kushirikisha RUWASA na kujiridhisha kuwa hali ya mitambo na miundombinu pamoja na idadi ya wateja waliopo vinaweza kuvutia Msimamizi Huduma/Mtoa Huduma na kuwa ushirikiano una uwezekano mkubwa wa kukidhi/kulinda maslahi ya pande zote mbili. RUWASA inaweza kutoa ushauri na kusimamia zoezi la kuunganisha Jumuiya ili kuongeza wigo na wingi wa wateja kwa minajiri ya kuweka mazingira ya kuvutia na kufanikisha ushiriki wa sekta binafsi.

(g) Maamuzi ya kushirikisha Sekta binafsi lazima yashirikishe wadau na Jamii husika katika mikutano halali kwa kuhakikisha wadau/wananchi wanaelewa umuhimu na faida za kushirikisha sekta binafsi. Maamuzi ya wananchi yatafanywa kwa azimio maalum litakalofikiwa katika mkutano na kuwekwa katika Muhtasari wa Kikao husika kwa kumbukumbu na rejea. RUWASA itawashirikisha wataalam na viongozi katika ngazi ya Halmashauri na Wilaya katika mchakato na hitimisho la zoezi hili.

(h) Baada ya kufikia uamuzi wa kushirikisha sekta binafsi, Mtoa Huduma au Msimamizi Huduma atakayechaguliwa lazima awe anakidhi viwango vya kuleta mabadiliko na matokeo tarajiwa. Baadhi ya sifa za Msimamizi Huduma/Mtoa Huduma zinaweza kuwa:-

(i) Awe amesajiliwa kisheria na vyombo husika na awe anafanya shughuli zake Tanzania

(ii) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu kwenye usanifu, ujenzi, ukarabati, usimamizi wa fedha, ushauri wa kiufundi na uimarishaji wa taasisi katika huduma za Maji na usafi wa mazingira hasa vijijini.

(iii) Awe na kipato ghafi kisichopungua shilingi za Tanzania milioni 150 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

(iv) Awe na vitabu vya taarifa za Fedha zilizokaguliwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyotangulia.

(v) Athibitishe kwa maandishi na Ushahidi kuwa ana timu ya watu wenye ujuzi, weledi na uzoefu wa kusimamia maeneo mbalimbali ya huduma na taasisi kama vile uendeshaji na matengenezo, ukusanyaji maduhuli na usimamizi wa fedha.

(vi) Awe na vitendea kazi au na uwezo wa kupata vitendea kazi muhimu katika shughuli atakazopewa kufanya kama vile mitambo ya huduma, machine/vifaa vya ofisi na usafiri/usafirishaji.

(i) Kama ni kikundi cha wataalam waliosomea fani ya maji watatakiwa wadhaminiwe na taasisi inayotoa huduma za maji jirani na eneo la Jumuiya inayokusudiwa. Dhamana itahusisha kuihakikishia Jumuiya kuwa wataalam hao wana ujuzi unaotakiwa na kuwa taasisi husika itawasimamia kuhakikisha ufanisi katika kazi na kuwa taasisi husika itawajibika kwa ubora na ubovu wa kazi itakayofanywa na wataalam hao.

## 6. HATUA ZA KUFUATA

Hatua zifuatazo zitazingatiwa katika kushirikisha Sekta Binafsi:

(a) Baada ya maamuzi ya kushirikisha sekta binafsi, tangazo litatolewa kukaribisha maombi ya wote wenye nia ya kushirikiana na Jumuiya husika katika kutoa huduma ngazi ya jamii. Tangazo litaeleza eneo, vigezo na sifa za waombaji pamoja na ukomo wa maombi. Tangazo litafafanua kama anatafutwa Msimamizi Huduma au Mtoa Huduma.

(b) Waombaji wanaweza kuwa Kampuni Binafsi, Asasi za Kiraia, Dhamana, Mamlaka za Maji au taasisi mahsusi za huduma za maji na usafi wa mazingira ili mradi usajili na shughuli zake ni Tanzania.

(c) Maombi yatakayopokelewa yatachambuliwa na kupata orodha ya waombaji wanaokidhi vigezo vya kuandaa andiko kwa utaratibu wa tenda.

(d) Waombaji wote watakaokuwa kwenye orodha ya waliokidhi vigezo watakaribishwa kwenye semina ya uelewa wa kazi inayotarajiwa kufanywa kabla ya kupewa makabrasha yatakayowawezesha kuandaa andiko la tenda. Semina itawahusisha pia Viongozi wa Jumuiya, Viongozi wa Jamii husika na wadau muhimu kutoka Wilaya na Mkoa husika.

(e) Baada ya semina waombaji wote watapewa makabrasha na maelezo ya namna ya kutayarisha na kuwasilisha andiko kwa muda utakaotolewa.

(f) Uchambuzi na uchaguzi wa waombaji utazingatia ushindani wa ubora wa maandiko yatakayowasilishwa na taarifa nyingine za uhalisia zitakazokusanywa nje ya andiko.

(g) Mwombaji atakayechaguliwa ndiye atakayeingia mkataba na Jumuiya husika kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yatakayoainishwa. Mkataba utaainisha masuala yote muhimu ikiwa ni pamoja na muda, fedha, notisi, taarifa, malalamiko, uendelevu na mahusiano.

(h) Jumuiya itaanzisha mfuko maalum wa Ukarabati na Upanuzi ambao fedha zake zitatokana na asilimia itakayolipwa na Msimamizi kwa kiwango kilichopangwa kwenye Mkataba na fedha kutoka Serikali na vyanzo vingine kupitia RUWASA.

## 7. MAJUKUMU YA MSIMAMIZI HUDUMA

Kimsingi, Msimamizi Huduma ana wajibu wa kusimamia utendaji wa kila siku wa Jumuiya na kuhakikisha kuwa huduma za maji na usafi wa mazingira zinaboreshwa na kuwa endelevu. Kwa muundo wa Jumuiya kwenye Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019, Msimamizi Huduma ndiye anachukuwa nafasi ya Timu ya Utendaji ya Jumuiya. Kimamlaka, shughuli zake zitasimamiwa na kutolewa taarifa kwa Kamati ya Maji.

Baadhi ya majukumu ya Msimamizi Huduma yanayoweza kuainishwa kimaandishi ni pamoja na :-

(a) Kusimamia shughuli zote za Jumuiya katika eneo husika kwa kuzingatia weledi na viwango vya huduma katika sekta ya maji. Atasimamia mitambo na miundombinu yote kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa bora na endelevu. Usimamizi sio tu unamaanisha kutekeleza makubaliano ya kimkataba kati yake na Jumuiya bali pia kutekeleza matarajio ya wateja wote wa kwenye virula na wale waliounganishwa majumbani.

(b) Kusimamia uendeshaji wa huduma na kufanya matengenezo ya kawaida ya miundombinu kwa gharama zitakazolipwa na mapato ya huduma anayosimamia. Matengenezo ya mara kwa mara na matunzo ya miundombinu ni muhimu kwa uendelevu wa huduma.

(c) Kufanya matengenezo ya kawaida ya mashine au kifaa chenye hitilifundani ya masaa ishirini nan ne (24) tangu hitilifu ilipotokea ili mradi gharama za matengenezo hayo ziko ndani ya viwango vyake kama ilivyoainishwa kwenye mkataba. Matengenezo yoyote ya mitambo, mashine na vifaa yanayozidi kiwango cha Msimamizi katika mkataba yatafanywa na Jumuiya kwa usimamizi wa RUWASA. Msimamizi atatakiwa kutoa maelezo ya kina ya gharama zinazotakiwa na gharama hizo zitalipwa kutoka kwenye mfuko wa Ukarabati na

Upanuzi kwa idhini ya RUWASA. Jumuiya na RUWASA wasiporidhika na maelezo ya malipo yanayotakiwa, Msimamizi atalazimika kulipa gharama husika kutoka kwenye mapato ya makusanyo ya tozo za huduma.

(d) Kuwajibika kukamilisha ukarabati wa mtambo, mashine au kifaa chochote kilichoharibika ndani ya masaa arobaini na nane (48) kuanzia siku alipopata taarifa rasmi ya ubovu huo.

(e) Kutoa taarifa ya kukatika kwa maji kwa sababu ya matengenezo yaliyopangwa au kwa dharura. Kwa matengezo yaliyopangwa atatoa taarifa kwa Jumuiya angalau siku mbili kabla ya siku ya kukatwa maji. Kwa dharura itakayosababisha maji kukatika kwa zaidi ya saa ishirini na nne atatakiwa kutoa taarifa ndani ya siku moja toka dharura ilipotokea na atatoa sababu iliyosababisha kukatika kwa maji na muda ambao huduma itarudi kwenye hali ya kawaida.

(f) Kutoa taarifa mapema kwa Jumuiya na RUWASA kuhusu ubadilishaji wa pampu na mitambo ya nishati pale ambapo muda wake wa kufanya kazi unapokaribia kikomo. Sharti hili la taarifa litahusu mitambo iliyopo wakati mkataba unapoanza na ile ambayo itanunuliwa baadaye wakati mkataba unaendelea.

(g) Kufanya tathmini ya kitaalam ya hali ya pampu na mitambo ya nishati ili kukadiria muda uliobaki wa kufanya kazi kwa mashine hizona hivyo kuwezesha kuwa na mpango mzuri wa uzalishaji wa maji bila kukatisha kwa kushitukiza.

(h) Kufanya mauzo ya huduma ya maji kwa wateja kwa kutumia dira ambazo zitakuwa sehemu ya makubaliano ya utoaji huduma. Dira zitakazotumika zitapimwa na maabara iliyoidhinishwa na RUWASA na zitafungwa kwenye maeneo ambayo ni rahisi kuzifikia na kuzikagua.

(i) Kuweka utaratibu wa kutunza na kulinda miundombinu ya maji isiharibiwe au kuibiwa kwa gharama zake za uendeshaji na matengenezo ya kawaida.

(j) Kutoa taarifa ya masuala ya uendeshaji, matengenezo na fedha kila mwezi kwa Jumuiya na RUWASA. Taarifa hiyo itajazwa kwenye fomu maalum itakayotayarishwa na itatakiwa iwasilishwe RUWASA kabla au kila ifikapo tarehe 10 ya kila mwezi unaofuata baada ya mwezi unaotolewa taarifa.

(k) Kuwasilisha mpango wa uwekezaji kila mwaka. Mpango huo utaelezea mapendekezo ya ukarabati, ubadilishaji wa vipuri na upanuzi wa mtandao wa huduma kwa mwaka unaofuata. Mpango huo utawasilishwa kwa Jumuiya na RUWASA katika robo ya mwisho ya kila mwaka isipokuwa mwaka wa kwanza wa mkataba ambapo Msimamizi wa Huduma atatakiwa kupeleka Mpango huo katika mwezi wa kwanza wa mwaka wa pili wa mkataba.

(l) Kuzingatia na kufuata masharti yote yaliyomo kwenye mkataba kuhusiana na ulipaji mrahaba, tozo na gharama zilizoainishwa. Aidha atazingatia vipengele vyote vya mkataba vinavyohusu uunganishaji wa maji majumbani na huduma kwa wateja.

(m) Kuwaruhusu RUWASA na Jumuiya kuingia na kukagua hali ya miundombinu na huduma wakati wowote ulioainishwa kwenye Mkataba ili mradi ukaguzi huo hauathiri utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa upande wa Msimamizi.

(n) Kuhudhuria na kushiriki katika kikao cha robo mwaka au kikao chochote cha dharura cha Jumuiya kwa taarifa na ukaribisho rasmi atakaopewa na Jumuiya. Msimamizi atatoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi husika. Nakala ya taarifa itakayosomwa katika kikao itapelekwa RUWASA.

(o) Kushirikiana na RUWASA na Jumuiya husika katika kufanya mapitio ya Mkataba wa uendeshaji wa mradi kila baada ya mwaka mmoja na kufanya maboresho ya mkataba pale itakapo onekana inafaa.

(p) Kutanguliza kiasi cha fedha sawa na asilimia ya gawio waliyokubaliana ya mwezi mmoja kabla ya kuingia mkataba, na atarejeshewa pindi Mkataba utakapo fika ukomo.

Mkataba utaainisha viwango vya gharama za matengenezo na uendeshaji ambavyo vitalipwa na Msimamizi Huduma na vile ambavyo vitalipwa na Jumuiya na/ au RUWASA kwa niaba ya Serikali. Viwango hivyo vitaonesha pia gharama za Msimamizi Huduma na Jumuiya katika matunzo na matengenezo ya mitambo, mashine na vifaa vya kuzalisha au kusambaza maji kama vile jenereta, pampu, tenki na bomba

## 8. MATARAJIO NA VIWANGO

Kwa vile sababu kuu ya kushirikisha sekta binafsi ni kuongeza ufanisi, kuimarisha ubora na kuhakikisha uendelevu wa huduma, Msimamizi wa Huduma anatarajiwa kupimwa uwezo wake kwa kuzingatia mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na :-

(a) Maji lazima yatoke katika virula na vichoteo vyote vinavyofanya kazi kwa muda wa saa ishirini na nne kwa siku saba kwa wiki. Muda halisi na saa za huduma itategemeana na eneo husika kwa jinsi ratiba itakavyowekwa kukidhi mahitaji na matakwa ya wateja.

(b) Wingi wa maji yanayotoka kwenye vichoteo vyote vya mtandao wa huduma lazima yawe na uwezo wa kujaza ndoo ya lita ishirini kwa dakika mbili.

(c) Iwapo mtandao wa maji hautakuwa na msukumo wa kufanya maji yatoke kwa nguvu iliayoainishwa hapo juu itachukuliwa kuwa ni udhaifu katika mtandao wa huduma na Msimamizi atatakiwa kushughulikia tatizo hilo kwa utaratibu ulioainishwa kwenye mkataba.

(d) Kuweka utaratibu na ratiba ya kukagua ubora wa maji angalau mara moja kila robo mwaka kwa kuzingatia vipimo na viwango vya ubora wa maji vya Tanzania. Msimamizi ataweka mitambo rahisi na rafiki ya kutibu maji.

(e) Kuhakikisha kuwa viwango vyote vya ubora wa huduma vilivyoainishwa kwenye Mkataba na viwango vyote vya kitaifa vinazingatiwa.

## 9. HAKI ZA MSIMAMIZI HUDUMA

Msimamizi wa Huduma atakuwa na haki zifuatazo:

(a) Kutumia mitambo, machine, miundombinu na vitendea kazi mahsusi kwa utoaji huduma na atakuwa na haki ya pekee kutoa huduma katika eneo la Jumuiya aliyoingia nayo mkataba.

(b) Kutumia ardhi iliyoko ndani ya mipaka ya eneo la huduma kwa ajili ya upanuzi wa huduma za maji.

(c) Kutoza huduma ya maji anayoitoa kwa wateja kwa viwango vya bei iliyokubalika katika mkataba na Jumuiya.

(d) Kuhamasisha na kuunganisha maji kwa wateja wa majumbani na taasisi kwa mujibu wa utaratibu ulioanishwa kwenye mkataba na Jumuiya.

(e) Kuunganisha na vile vile kukata huduma kwa wateja wasiolipa kwa utaratibu ulioainishwa kwenye mkataba.

(f) Kulipwa fidia ya kukatisha mkataba wa kutoa huduma kwa masharti na viwango vitakavyoainishwa kwenye Mkataba.

## 10. WAJIBU NA HAKI ZA RUWASA

RUWASA ndiye mwangalizi mkuu wa mkataba wa ushirikiano na mahusiano baina ya Sekta binafsi na Jumuiya. Katika mukhtadha huo RUWASA,

(a) Itapitia mipango na taarifa za utekelezaji za Msimamizi wa Huduma pamoja na kuhoji na kuingilia kati vitendo au mwenendo unaotishia ukiukwaji wa mkataba na misingi ya ushirikishaji wa sekta binafsi.

(b) Itatenga bajeti na muda wa kutosha kwa minajiri ya kusimamia kwa ukaribu na ukamilifu ufanisi wa ushirikiano huu.

(c) Haitaingilia bila sababu maalum utendaji wa Msimamizi wa Huduma isipokuwa katika vipengele ambavyo vimeainishwa kwenye mkataba.

(d) Itatoa ushirikiano na kumpa Msimamizi nafasi ya kuona na kupata taarifa, mipango, sera, sheria na takwimu zozote zitakazosaidia kuongeza ufanisi katika huduma. Aidha itamwezesha Msimamizi wa Huduma kupata vibali na leseni zote zinazotakiwa kisheria ili huduma iwezo kutolewa kwa misingi ya Sera, Sheria, Taratibu na Miongozo husika.

(e) Itasaidia kuweka sawa na kufanya suluhu kati ya Jumuiya na Msimamizi wa Huduma pale itakapobidi na itafanya chochote ndani ya mipaka ya Sera na sheria kitakachosaidia kuimarisha uhusiano na huduma za maji na usafi wa mazingira.

(f) Itaandaa mkataba utakao ingiwa kati ya Jumuiya za Huduma ya Maji Ngazi ya Jamiii na Mtoa Huduma/Msimamizi mradi

(g) Itaingia mkataba na Mashirika/watu binafsi kuanzisha na kuiendesha miradi ya maji na kugawana mapato kwa asilimia (%)

(h) Kwa kushirikiana na Mtoa huduma/mwendeshaji na Jumuiya husika, kufanya mapitio ya Mkataba wa uendeshaji wa mradi kila baada ya mwaka mmoja na kufanya maboresho ya mkataba pale itakapo onekana inafaa.

(i) Kusimamia uandaaji na ulipwaji wa mgao (%) unaorejeshwa kutoka kwa msimamizi kwenda kwa CBWSOs.

(j) Kukagua mapato na matumizi ya fedha kwa mujibu wa sheria na taratibu za fedha.

(k) Kuthibitisha ubora wa maji kulingana na viwango vya ubora wa maji vilivyopo.

## 11. MAJUKUMU NA HAKI ZA JUMUIYA

Majukumu na haki za Jumuiya ni pamoja na:

(a) Kutokuingilia utendaji kazi wa Msimamizi au Mtoa Huduma wakati wa utekelezaji wa majukumu yake yaliyoainishwa kwenye Mkataba. Aidha haitafanya vitendo vitakavyochagiza uharibifu wa mitambo, mashine na miundombinu ya maji na watahamasisha wananchi kuleta na kutunza miundombinu na mazingira husika.

(b) Kurekebisha kwa gharama za Jumuiya, uharibifu wowote utakatokana na kitendo au mwenendo wa Jumuiya kwa kupitia viongozi au wanachama wake.

(c) Kusaidia na kumwezesha Msimamizi wa Huduma katika kuhudumia wateja kupitia kwenye Virula, majumbani, ulipaji wa Ankara za maji na usikilizaji wa malalamiko.

(d) Kutoa taarifa na takwimu muhimu zitakazoiwezesha RUWASA kufuatilia na kusimamia na kutathmini vema utendaji wa Msimamizi wa Huduma.

(e) Kubaki na mamlaka ya kushirikishwa na kuidhinisha kuunganishaji wa maji kwenye mabomba binafsi na taasisi.

## 12. UKOMO WA MWONGOZO

Mwongozo huu utadumu sambamba na ukomo wa RUWASA bila kuathiriwa na mabadiliko ya maudhui au vipengele ndani ya Mwongozo. Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA anaweza kutangaza ukomo wake kutakapokuwa na mbadala wa kuongoza na kuelekeza masuala yote ambayo yanabeba lengo la Mwongozo huu.

## 13. KUPITISHWA

**Tarehe:** 24/06/2020

**Saini:** [signature]

**Jina:** PROF. IDRIS A. BILALI MSHORO

**Cheo:** MWENYEKITI WA BODI

**Muhuri:**